## Maswali

1. Paulo alijuaje kwamba Mungu anataka aende Makedonia?
2. Paulo na Sila walienda kwa mji gani?
3. Paulo alihubiri wapi? Nani aliamini na akabatizwa?
4. Nani alikuwa akifuata fuata Paulo?
5. Mbona wenye mjakazi wa pepo walikasirika?
6. Waamuzi walifanyaje Paulo na Sila?
7. Paulo na Sila walifanya nini usiku wa manane?
8. Nini ilifanyika usiku wa manane?
9. Mbona mlinzi wa gereza alitaka kujiua?
10. Mlinzi wa gereza na familia yake walifanya nini usiku wa manane?

## Majibu

1. Katika ndoto zake alisikia mtu akimwiita, “Kuja huku Makedonia na utusaidia.
2. Paulo na Sila walienda Makedonia.
3. Nje ya mji kwa ukingo wa mto. Lidia aliamini na akabatizwa.
4. Mjakazi. Alikuwa na pepo. Alikuwa muaguzi wa watu wake.
5. Paulo aliponya yule mjakazi. Hangeweza kuagua kwa sababu alikuwa amepona. Watu wake walipotesa pesa nyingi.
6. Waamuzi waliwapiga Paulo na Sila na kuwaweka gerezani.
7. Paulo na Sila waliomba Mungu na kuimba nyimbo za sifa.
8. Kulikuwa na mtetemeko wa ardhi. Milango ya gereza ilifunguka. Wafungwa walifunguliwa minyororo.
9. Mlinzi alifikiria kwamba wafungwa wote walikuwa wametoroka
10. Walimsikiliza Paulo akiwambia habari ya Yesu. Waliamini Injili. Walibatizwa.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 2    Mwaka wa 2**

# 96 Paulo na Sila gerezani

### Kwa Biblia

Matendo ya Mitume 16 : 6 – 40

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Paulo na Sila walifurahi sana kumtumikia Mungu hata kama walikuwa kwa shida

### Somo

Paulo alikuwa akihubiri Injili. Alikuwa ana safari na rafiki yake Sila. Walipitia pwana mpaka Troa. Paulo alijiuliza, ni wapi ataenda kuhubiri Injili. Usiku huo Paulo alikuwa na ndoto. Aliona mtu ng’ambo ya bahari akitoka Makedonia. Yule mtu aliita Paulo na kusema, “Kuja huku Makedonia na utusaidie.” Hapo Paulo alijua kwamba Mungu alitaka waende wahubiri Injili kwa nchi ya Makedonia. Paulo na Sila walivuka ng’ambo mpaka Makedonia.

Paulo na Sila walienda Filipi. Filipi ulikuwa mji wa Kirumi. Askari wengi wa kirumi waliishi hapo. Filipi ulikuwa ni mji wa shuguli nyingi. Ulikuwa karibu na pwani. Watu wengi walikuja hapo kufanya biashara. Hapo Filipi hakukuwa na Wayahudi wengi, kwa hivyo hakukuwa na Sinagogi ya kukutania. Wayahudi walikutania nje ya mji kwa ukingo wa mto.



Paulo na Sila walienda ukingoni mwa mto kila siku ya Sabato. Waliambia Wayahudi juu ya Yesu. Baada ya muda mwanamke aitwae Lidia aliamini. Lidia alikuwa mfanyi biashara. Alitoka kwa mji wa Thiatira uliokuwa umejulikana kwa rangi za zambarau. Lidia aliuza nguo za zambarau.

Paulo alihubiri Injili kwa watu wa Filipi. Alikutana na kijakazi mmoja aliyekuwa na pepo. Huyu mjakazi aliletea watu wake pesa nyingi sana kwa uaguzi wake. Huyu mjakazi akafuata Paulo na Sila. Akipiga kelele akisema, "Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliyejuu. Wanamwambia vile mnaweza kuokoka." Paulo hakutaka Injili ichanganyikiwe na uaguzi wa msichana huyu. Siku moja Paulo akageuka na kumponya huyo mjakazi.


Wenye huyo mjakazi walikasirika sana. Mjakazi huyu hangeweza kuwaletea faida tena kama mwanzoni. Watu wake wangepotesa pesa nyingi kwa sababu alikuwa ameponywa. Watu wake wakachukua Paulo na Sila mpaka sokoni mbele ya waamuzi. Watu wengi walikusanyika pale. Kila mtu alipigia Paulo na Sila kelele.

Waamuzi waliwapiga Paulo na Sila na kawaweka gerezani. Mlinzi wa gereza aliambiwa kuwachunga sana. Mlinzi aliwaweka chumba cha ndani sana gerezani. Alifunga miguu yao kwa mikatale. Paulo na Sila walikuwa na baridi bila raha kule gerezani. Migongo yao ilikuwa na vidonda ikitokwa kwa damu kwa ajili ya kupigwa.

Paulo na Sila hawakuwa wakijifikiria wenyewe. Hawakujihurumia. Walijua Yesu alikuwa ameteswa msalabani kwa ajili yao. Walifurahi kuumia kwa ajili yake.

Waliomba Mungu. Katikati ya usiku waliimba nyimbo za kumsifu Mungu. Wafungwa wengine waliangalia kwa mshangao. Hawakuelewa kilicho endelea. Paulo na Sila walikuwa wamepigwa na kutupwa gerezani. Walisikia baridi na kuumwa. Lakini bado walikuwa wanaimba sifa kwa Mungu!

Mungu alikuwa anasikiliza Paulo na Sila wakiimba nyimbo za sifa. Mungu alifurahia hiyo imani yao. Bunde tu, kukawa na mtetemeko wa nchi. Mizingi ya gereza ilitingika. Milango za gereza zikafunguka. Minyororo za wafungwa zikafunguka. Mlinzi wa gereza akaamka na kuona milango yote iko wazi. Alitaka kujiuwa kwa sababu alifikiri kwamba wafungwa wote wametoroka. Paulo akapaza sauti akasema, "Usijiuwe! Sisi wote tuko hapa."



Mlinzi wa gereza alishangaa kwa sababu ya imani ya Paulo na Sila. Akapiga magoti mbele ya Paulo na akasema, "Nifanye nini ili niokoke?" Walimjibu, "Amini kwa Bwana Yesu, wewe na familia yako yote na mtaokoka?"

Mlinzi wa gereza alichukua Paulo na Sila mpaka nyumbani kwake. Paulo aliambia mlinzi wa gereza pamoja na familia yake habari ya Yesu na wakaamini. Mlinzi aliosha vinonda vya Paulo na Sila. Halafu mlinzi na familia yake wakabatizwa papo hapo – usiku wa manane. Aliwapa chakula. Huyo mlinzi na familia yake walifurahi kwa sababu walikuwa na imani kwa Mungu na walikuwa wakristo sasa.

Ilipofika asubuhi, waamuzi walisema Paulo na Sila waachiliwe. Walijua hawakuwa wamewafunga kwa haki. Paulo aliwatumia ujumbe kuwambia kwamba yeye alikuwa Mrumi. Ilikua hatia kumfunga Mrumi bila kumhukumu kwa haki. Waamuzi waliona kwamba wako kwa hatari kubwa. Waamuzi walienda ndani ya gereza na kuomba Paulo na Sila msamaha. Waliwaleta nje ya gereza. Waliuliza Paulo na Sila kuondoka mjini ili kusitokee na shida ingine. Paulo na Sila walipea Lidia kwaheri na kuondoka.